

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Indonesia
25 Januari, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AFANYA ZIARA YA SIKU MBILI NCHINI INDONESIA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Indonesia wameshuhudia makabidhiano ya Hati za Makubaliano 4 na barua ya kusudio 1 kati ya nchi hizo mbili.

Rais Samia akizungumza na waandishi wa habari katika ziara ya Kitaifa nchini humo amesema makubaliano hayo yataimarisha miaka 60 ya kidiplomasia na uchumi.

Miongoni mwa masuala waliojadili viongozi hao ni namna ya kuimarisha uhusiano wa kibiashara na uwekezaji ambapo Tanzania ipo tayari kuwa mwenyeji wa mkutano wa kwanza wa tume ya Makubaliano ya ushirikiano.

Pia kumekuwa na majadiliano ya namna ya kuendeleza ushirikiano katika uwekezaji kwenye sekta ya mafuta na gesi huku kampuni ya Indonesia ya Pertamina ikiongeza hisa Mnazi Bay, Mtwara.

Mbali na kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa TPDC, pia Indonesia ina nia ya kampuni yake ya ESSA kuwekeza kwenye kilimo hususan mbolea na Medco Energi kwenye upande wa nishati.

Kwa upande wa sekta ya dawa, kipaumbele hasa ni Indonesia kuiuzia Tanzania dawa ambapo kwa kuanzia zitakuwa za saratani.

Makubaliano mengine 3 ambayo Rais Samia ameshuhudia ni pamoja na Uchumi wa Buluu, ushirikiano wa sekta ya kilimo, madini, diplomasia biashara na elimu ya juu.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Zuhura Yunus'.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

